NISHANI YA HIKING

SOUTHERN HIGHLAND CONFERENCE

IDARA YA HUDUMA ZA VIJANA

KANISA LA WAADVENTISTA WA SABATO
IDARA YA HUDUMA ZA VIJANA
EDITED BY: MASTER: YUSUPH LUCAS MWASIPOSYA

NISHANI YA HIKING

HIKING NA MAHITAJI YAKE.

Nishani hii ipo katika kundi la maburudisho na michezo, huwakilishwa kwa rangi ya kijani

Hiking ni moja ya hitaji katika vyama vya vijana kanisani na ni sehemu ya maburudisho.

Hiking ni nini? Kuna maana nyingi za hiking, hiking ni neno la kiingereza linalotokana na neno "Hike"

Maana ya Hiking: -Ni kitendo cha kutembea mwendo mrefu au mfupi kwa kufuata alama na kwa makusudi maalum katika mazingira ya asili mara nyingi katika maeneo ya milima.

Makusudi hayo yanaweza kuwa

i. Kufanya Mazoezi
ii. Kujifurahisha
iii. Utambuzi.

Matembezi hayo yanaweza kuwa ya siku moja ambayo hayahitaji kambi ya usiku mzima, au ya siku nyingi yanayohitaji ukambikaji ambayo kwa maeneo mengine yanajulikana kwa jina la "Trekking"na sehemu nyingine "Thru-hiking".

Kuna alama nyingi za njiani pia za kutafuta vitu vilivyopotea. Alama hizi hutumiwa na vijana wa A.Y, P.F.C na A.C. Pia hutumiwa na madreva pamoja na scout kwa makusudi ya kufika pale watakapohitaji kufika-mfano wa nyota iliyowaongoza Mamajusi injili za Luka, Mathayo husimulia.

- Kwa mara ya kwanza Adamu ndiye mwanadamu wa kwanza kushiriki nishani hii ya hiking katika uumbaji, hii huelezwa kutoka katika kitabu cha Mwanzo katika suala zima la uumbaji.

Yapo mambo mbalimbali pamoja na ishara zinazochorwa kuelezea hali halisi ya eneo husika-alama za mishale → ☐ , mraba ▭,msitatili ⬭ ,duara △ ,pembe tatu ☆ , na herufi mbalimbali tofauti na umbile la nyota lililowaongoza Mamajusi.

Alama hizi huchorwa kwenye vibao, zingine huchorwa njiani juu ya ardhi ili kuongoza wapitaji husika wapate kufika sehemu wanayotakiwa au kupata kile kilichokusudiwa na jamii husika.

Alama hizi pia huweza kutumia miti, matawi ya miti, hata mashina ya miti pia na wakati mwingine mawe hutumika na inapolazimu nyasi na vichaka hutumika.

Katika alama hizo ziwe njiani au porini huonyesha uelekeo, hali ya hatari, hali ya usalama na jinsi watu wake walivyo na vitu gani ni hatari katika maeneo husika.

AINA ZA HIKING.

Zipo aina nyingi za Hiking nyingi zikitegemea kusudi halisi na lengo la matembezi hayo nap engine kutegemea muda wa matembezi hayo.

1.HIKING KULINGANA NA KUSUDI AU LENGO LA MATEMBEZI HAYO.

- SKILL HIKE: -Ni aina ya Hiking ambayo lengo kubwa ni utambuzi wa vitu (Kitendo cha kutembea kwa kugundua vitu Fulani)
- COMMUNICATION HIKE: -Kitendo cha kutembea kwa kugundua alama za mwenzako.
- FRIEND TO MEN HIKE: -Kuwatembelea ndugu na jamaa kwa kusudi maalumu kwa mfano: -Hospitalini, kwenye misiba, harusi n.k
- NATURE BIBLE TREASURE HIKE: -Kutembea kwa makusudi ya kupeleka ujumbe.
- LOST CHILD HIKE: -Kutembea kwa ajili ya kumtafuta mtoto aliyepotea.
- FIRST AID HIKE: -Kutembea kwa ajili ya kwenda kutoa huduma ya kwanza.

2.HIKING KULINGANA NA MUDA WA MATEMBEZI HAYO.

- ✓ TREKKING HIKE (MULT DAY): -Pia hujulikana kama “BACKPACKING” haya ni matembezi yanayochukua siku zaidi ya moja na mara nyingi hufanyika sehemu za milimani

- ✓ A DAY HIKE: -Ni matembezi yanayofanyika na kumalizika ndani ya siku moja, na yasiyohitaji kambi ya usiku kucha.

3.HIKING KULINGANA NA MAZINGIRA /MAENEO YA MATEMBEZI.

- ❖ HELI HIKING: -Matembezi kwa njia ya Helicopita au ndege kufikia maeneo magumu yasiyofikika kwa njia nyingine yeyote.
- ❖ BUSWHACKING(DAYHIKING): -Matembezi kupitia maeneo magumu ya vijijini kwa kutumia ramani.
- ❖ HILLWALKING: -Matembezi katika vilima na milima mbalimbali.
- ❖ WATERFALL HIKE: -Matembezi kwa kugundua na kupitia maeneo mbalimbali ya maporomoko.

4.MATEMBEZI KWA KUTUMIA VIUMBE VYA ASILI.

- DOG HIKING: -Matembezi kwa kutumia mbwa.

MAKUSUDI YA HIKING.

Kuna makusudi mengi ya Hiking kulingana na mahitaji ya matembezi husika na yafuatayo ni baadhi ya makusudi au umuhimu wa hiking: -

- Kuwazoeza vijana kuwa wakakamavu.
- Kukuza moyo wa udadisi.
- Kujifunza ukuu wa Mungu.
- Kujenga moyo wa ujasiri na kujiamini.
- Kukuza ushirikiano kati ya vijana.
- Kujifunza jiografia kwa kupanua mazingira.
- Kujenga urafiki na kufahamiana.
- Kukuza kipawa cha uongozi.
- KIAFIYA

  -Kupunguza uzito kutokana na matembezi ambayo yanahusisha mazoezi.

  -Kupunguza msukumo wa damu (blood pleasure-bp)

-Inasaidia kuzuia ugonjwa wa udhaifu wa mifupa(Osteoporosis) kwa kuimarisha mifupa.
-Kuondoa maumivu ya mgongo.

- Kujiandaa kwa ajili ya tabu ya Yakobo.

TABU YA YAKOBO.

Yeremia 30:7-Ole! Maana siku ile ni kuu, hata hapana inayofanana nayo, maana ni wakati wa taabu yake Yakobo; lakini ataokolewa nayo.

Katika kitabu cha “Confilct and Courage” cha Ellen G. White sura ya 62 anaeleza: - ***“Ole! Maana siku ile ni kuu, hata hapana inayofanana nayo, maana ni wakati wa taabu yake Yakobo; lakini ataokolewa nayo.”***

Wakati kazi ya Yesu itakapokoma kama mpatanishi kati ya mwanadamu, ndipo wakati huu wa taabu itakapoanza. Ndipo hukumu ya kila nafsi itakapokuwa imeamuliwa na hakutakuwa na damu ya kutakasa dhambi tena.

Na tena Roho wa Mungu ataondolewa kutoka katika dunia hii. Kama Yakobo alivyotishwa kwa mauti na ndungu yake mwenye hasira; hivyo ndivyo watu wa Mungu watakavyokabiliwa na hatari toka kwa waovu wanaotafuta kuwaangamiza. Na kama mzee Yakobo alivyopigana/pambana mieleka usiku kucha ili akombolewe toka katika mikono ya Esau, hivyo ndivyo watakatifu watakavyomlilia Mungu Mchana na Usiku kwa ajili ya ukombozi wao kutoka kwa maadui wale watakaowazunguka…

Wakati wa utambuzi wake Yakobo aliendelea kumshikilia Malaika na akafanya maombi ya unyenyekevu kwa machozi,mjumbe kutoka mbinguni ,katika kumjaribu imani yake,pia kumkumbusha dhambi zake,na akajitahidi kumkwepa Yakobo.Lakini Yakobo asingegeuka mbali(hakumwacha).Yeye alishajifunza kwamba Mungu ni Mungu wa Rehema,naye akajitupa mwenyewe juu ya Rehema zake.Akakumbuka maungamo ya dhambi zake,na akaomba ukombozi.Alivyotathimini maisha yake akajikuta yu katika hali ngumu ya kukata tama,lakini alimushika Malaika kwa haraka,na kwa bidii,maumivu makali alilia na kusihi mpaka aliposhinda.

Hivi ndivyo uzoefu wa watu wa Mungu utakavyokuwa katika pambano lao la mwisho dhidi ya nguvu za uovu.Mungu atajaribu imani yao,uvumilivu wao na ujasiri wao katika nguvu zake za kuwakomboa.Shetani atawajaribu kuwatisha wao na mawazo ya kwamba kesi yao haina matumaini;ya kwamba

dhambi zao ni nyingi kiasi kwamba haitasamehewa.Watakuwa na hisia ya kina kuhusu mapungufu yao,na kwa jinsi wanavyotathimini maisha yao tumaini lao ya dhati.Wakati Ahadi zake kupitia Kristo pasipo msaada,wadhambi walioungama.Imani yao haitashindwa ati kwa sababu tu maombi yao haikujibiwa mara moja.Wataendelea kushikilia nguvu za Mungu,Kama Yakobo alivyomshikilia Yule Malaika,na lugha ya Mioyo itakuwa “Sitakuacha uende mpaka umenibariki”

MAANDALIZI YA HIKING.

Kwanza kabisa ni bora kufanya mjadala na wanahiking kabla ya kuanza hiking yenyewe ili kuelewa nia dhumuni na lengo la kufanya hiking hiyo na manufaa yake kwa wanahiking.

Pili kuamua ni wapi mtakapokwenda kwa ujumla, ama sehemu za milimani au miteremko mikali ama baharini au sehemu za tambarare na kama kuna lengo au kusudi lolote la kwenda huko. Eneo husika la kituo cha mwisho cha hiking ni jukumu la kiongozi kulifahamu vizuri.

Je, mnakwenda kutembea tu au kufanya ziara mahali Fulani kwa lengo maalum.

Wakati haya yakishajadiliwa utapaswa kama kiongozi kuandaa mpangilio wa njia zote mtakazopita na kutoa mpango mzima wa njiia.

Mara tu njia na kusudi la hiking hiyo likishafikiwa ndipo yapaswa kutoa taarifa na kuomba ruhusa kwa wazazi au walezi wa wana hiking waliokusudiwa kama inawezekana basi maombi hayo yawe katika maandishi.

Punde mfikiapo karibu na siku yenyewe ya Hiking unahitajika kukusanya vifaa vyote, na kuangalia kama vinafaa na vinafanya kazi vizuri kuviweka vizuri. Na wote waliokusudiwa kwenda hiking wana vifaa vyote vinavyohitajika.

MAHITAJI MUHIMU YA HIKING/VIFAA VYA HIKING.

Katika kufanya hiking vifaa vinavyohitajika hutegemea na ni wapi unakwenda, ni kipindi gani cha mwaka (masika au ukame), aina, urefu na chanzo cha hiking husika. Hata hivyo Vifaa vifuatavyo vinapaswa kuandaliwa mapema toka kwa kila kijana na vikaguliwe kabla ya safari haijaanza.

I. GONGO: -Liwe lenye unene ambao mkono utaweza kulishika vizuri na liwe na urefu usawa wa bega lako unapolitembelea.

Matumizi ya gongo.

a) Kutembelea na kukupa support/muegamo katika sehemu za milima kupanda na kuteremka kwa urahisi.
b) Kuruka katika sehemu za vijito vidogo vidogo na sehemu za vizuizi pia.
c) Hutumika kama silaha na kinga: -kuuwa wadudu wenye sumu kama nge, tandu, nyoka n.k
d) Hutumika katika huduma ya kwanza mfano, mtu akivunjika au kuteguka mguu, pia kama machela kwa Yule atakayelemewa na safari au kushambuliwa na kitu chenye sumu n.k
e) Hutumika kama daraja katika kuvuka vijito.
f) Hutumika kama nyenzo ya kuvuta wengine katika sehemu zenye magema. (escarpment/cliff).

II. KAMBA NDEFU NA IMARA.

- Huwezesha watu wapite sehemu ngumu au zisizoweza kupitika kwa urahisi.
- Hutengeneza machela.
- Kubeba vitu mfano kidumu cha maji.
- Hutumika kufungia mafundo mbalimbali tukiwa porini.

III. SKAFU.

- Katika sehemu zenye baridi huvaliwa shingoni ili kuongeza joto.
- Ikiwa kuna uhaba wa Kamba skafu yaweza kutumika katika huduma ya kwanza kwa aliyeumwa na nyoka kwa njia ya kufunga juu ya jeraha ili, sumu isisambae kwa urahisi mwilini.
- Hutumika katika matumizi mbalimbali katika maeneo yenye joto kali na vumbi jingi pia kama mkanda katika sketi na suruali.
- Hutumika pia katika michezo mbalimbali.

IV. MAJI

- Pasipo maji ya kutosha, misuli ya mwili wako na viungo vya mwili haviwezi kufanya kazi kwa uzuri; unaweza kukabiriwa na kiu kali na uchovu mwingi(hyporthemia).
- Kuanzia lita tatu na kuendelea, hunywewa mahali maalumu kwa ruhusa ya kiongozi wa kundi lenu wakati wa hiking au mahali mulipoelekezwa kufanya hivyo.

V. CHAKULA.

- Kile ambacho si rahisi kuharibika au kuvunda na kiwe cha kubebeka kwa urahisi. Viwe vya jamii ya nafaka ya ngano mfano;
- Mikate, skonzi, chapati, mabumunda, nap engine juisi na matunda kama ndizi.

VI. MAVAZI.

- Yawe imara yasiyobana na kutatuka kwa urahisi.

VII. VIATU.

- siyo ndala au Yebo, viatu vya kuchomeka au vile vya nylon visibane au kupwaya mno.

VIII. VIFAA VYA HUDUMA YA KWANZA.

- Wembe, bandage, sindano au pini n.k

IX. BIBLIA, KITABU CHA WIMBO, DAFTARI NA KALAMU.

X. KUWEPO NA SANDUKU LA HUDUMA YA KWANZA KILA KIKOSI.

XI. RAMANI KAMA IKIWEZEKANA KWA KIONGOZI ANAEANDAA WAKATI WA MAANDALIZI ILI KULIELEWA ENEO VIZURI ZAIDI.

XII. DIRA-Dira yaweza kuwa msaada kukusaidia kutafuta njia ya sehemu ya nchi usiyoijua au madhari usiyoyajua kata maeneo ambayo hali ya hewa ni mbaya ambapo huwezi kutafuta alama za uoto wa asili kwa urahisi.

XIII. KIWASHIA MOTO AU KIBERITI-moto ni msaada mkubwa kwa ajili ya alama pindi unapokuwa uumepotea.

XIV. KUWEPO NA FILIMBI ZITAKAZOTUMIKA KULINGANA NA VIKOSI VILIVYOPO.

- Milio ya filimbi hutusaidia pale tunapokuwa katika mkusnyiko wa jamii

  kama vile kambini, michezoni n.k

- Milio ya Filimbi imegawanyika katika sehemu kuu mbili ambazo ni; -

  - 1. Mlio mrefu (________)

  - 2. Mlio mfupi (.   )

Ni juu ya kila mwanachama wa chama cha watafutanjia kujua ni nini maana ya milio hiyo, na pia aelewe pia ni kwa jinsi gani atekeleze amri hiyo.

Hebu tuone baadhi ya milio hiyo ya Filimbi

"**_________**" Inamaanisha uwe tayari, uwe macho, angalia au sikiliza.

". . . . ." Inamaanisha wote njooni.

". . .__. . .__." Inamaanisha viongozi wote, njooni.

".___. ____." Kuna hatari, mjihadhari (help or Surrender).

"__ __   __" Tawanyikeni, endeleeni na shughuli zenu.

Milio hii hutumika maeneo mengi yakiwemo, maeneo ya Kijeshi, scout, vijana kanisani kikiwemo chama cha watafutanjia, muhimu ni kuelewa ni kwa namna gani milio hii hutumika hasa

Nyakati za mikusanyiko ya vyama mbalimbali kanisani, kama vile upandishaji wa bendera ya chama na hata ya vyama mbalimbali kanisani.

SHERIA ZA HIKING

1. Shika Gongo usawa wa nyuzi 45^o
2. Usile chochote njiani mpaka kwa ruhusa maalum.
3. Usitembee huku unakunywa safarini. Kama una kiu weka jiwe dogo(pebble) mdomoni na endelea kulimung'unya.
4. Pumua kwa kutumia pua na si mdomo.
5. Uwe mtii na mwenye nidhamu uwapo safarini.
6. Usitembee haraka sana kiasi cha kuwaacha wenzako wala usiwe nyuma sana kiasi cha kujitenga na wenzako.
7. Usimkanyage aliye mbele yako wala kuburuza miguu.
8. Tembea katika mstari mmoja/kufuata safu moja. (singlefile)
9. Angalia gari lililombele yako. Pita kulia mwa barabara.
10. Usicheleweshe Habari ulizopewa kuzipeleka nyuma au mbele yako.
11. Pumzika baada ya dk.50 kwa dk.10 kufanya dk.60
12. Kiongozi ahakikishe kwamba hakuna mwana Hiking aliye bakia nyuma.
13. Milio ya filimbi ndiyo ishara ya amri zote.
14. Ni bora kuvaa sare.
15. Hakikisha unafahamu umbali unapotembea hii yaweza kukusaidia upoteapo au kukadiria muda maana kuna maeneo ambayo huwezi kuruhusiwa kupita inapofika muda Fulani.
16. Hakikisha unachakula cha kutosha kwa ajili ya tahadhali maana huwezi jua mwisho hadi umalizapo safari yako na kurudi nyumbani salama. Na hakikisha usile matunda yoyote porini kwenye miti hata kama utakuwa na njaa kiasi gani.
17. Kama utahisi umepotea rudi kwenye alama ya mwisho uliyofikia, mwombe Mungu kasha endelea na safari.
18. Kama utahisi kupotea kabisa, tengeneza moto wa ishara ili wenzako wakiona moshi waje wakusaidie au puliza filimbi ya hatari mara tatu mfululizo kwa pumziko fupi.

MOTO NA MATUMIZI KATIKA HIKING.



i.Kambi liko hapa ii. Nimepotea nisaidieni. iii.Kuna habari njema.

19.Kumbuka kuchora ramani mara baada ya kurudi kituoni.

KUCHORA RAMANI YA HIKING.

Ili kupata nishani ya Hiking, Sehemu ya maana na yenye maksi nyingi ni kuchora Ramani zingatia yafuatayo: -

i. ELEWA UELEKEO: -Kama ni kaskazini, kusini, magharibi au mashariki.
ii. Elewa vituo vyote mlivyopumzika.
iii. Elewa miti mliyovuka kama ipo.
iv. Elewa sehemu mlizopita kama ni shamba, kijiji, shule, msikiti, makanisa, nguzo za simu, reli n.k
v. Elewa alama zinazochora kusimama badala yake, kwa mfano: -

a.  Huonyesha daraja.

b.  Huonyesha reli.

c.  Huonyesha milima na mabonde.

d.  Huonyesha Kanisa

e.  Huonyesha msikiti.

f. N. B Kuna vitabu vya jiografia vingi mashuleni katika shule za msingi na sekondari ambavyo huonyesha alama nyingi. Utafanya vyema kujifunza alama hizo ili uelewe na kufuzu nishani hii ya Hiking vizuri na iwe na manufaa katika maisha yako wewe kama kijana.

ALAMA ZA MSITUNI.

Kama tulivyokwishaona kwamba Hiking ni kutembea mwendo mrefu au mfupi kwa kufuata alama. Mara nyingi kutembea Hiking, hatutembei kufuata barabara au njia za watu, bali tunatembea porini kwa kufuata alama maalum.

Katika eneo kama hili la msitu mara nyingi hutumia alama za miti kwa aina zake nap engine hata vichaka na pale inapolazimu hutumia mawe na hata michoro pia.

MASHARITI YA UWEKAJI ALAMA.

i. Viongozi wote wanapaswa kulitembelea eneo watakaloelekea mapema na ikibidi waweke alama zitakazofuata, mapema kabla ya siku kufika.
ii. Hakikisha hakuna mtu mwingine anayekuona unapoweka alama hizo, maana naweza kuzivuruga na kupoteza vijana.
iii. Hakikisha hakuna alama nyingine inayofanana na alama yako, isije ikawapoteza wana hiking.
iv. Wale wanaokuja nyuma wahakikishe wanazifuta alama hizo ikiwa hakuna mwingine nyuma yao.

Kuna aina mbalimbali za alama kama ifuatavyo: -

Ziko alama za miti, mawe na nyasi pia na michoro, Kiongozi uhakikishe wanahiking wamefundishwa vyema na kuzielewa alama hizo vizuri kabla ya kufanya hiking yoyote.

SANDUKU LA HUDUMA YA KWANZA.

Ni jambo la muhimu kuwa sanduku la huduma ya kwanza, mnapoelekea kwenye Hiking au kwenye kambi, ni vizuri sanduku hilo liwe la miti, mbao, au plastic kuliko la bati maana hilo hushika kutu.

MGAWANYIKO WA SANDUKU LA HUDUMA YA KWANZA.

-Sanduku la huduma ya kwanza lapaswa ligawanyike sehemu muhimu tatu.

a. SEHEMU YA KWANZA- sehemu ya kuweka aina mbalimbali za vidonge kama Asprini, Panadol n.k
b. SEHEMU YA PILI: sehemu ya kuweka dawa za majimaji kama jivii, spiriti, salimia n.k
c. SEHEMU YA TATU- sehemu ya kuweka mkasi, bandage, wembe n.k

-Kwa kawaida sanduku hili hutunzwa na mtu maalum aliyechaguliwa na kuelekezwa namna ya kutumia vifaa hivi vya huduma ya kwanza kwa kila kikosi cha wana hiking.

YAMPASAYO MTOAJI HUDUMA YA KWANZA.

i. Awe na ujuzi kamili au mafunzo maalumu, ni bora wana hiking wakafundishwa nishani ya huduma ya kwanza kabla, ili asiifanye kazi hii kwa kubahatisha.
ii. Alitunze sanduku katika hali ya usafi.
iii. Dawa zifungwe vizuri. Zisiingize hewa
iv. Awe mpole na mwenye kuwahurumia wagonjwa.
v. Awe na lugha nzuri yenye matumaini nay a kufariji wagonjwa.
vi. Awe mwepesi kuona na kugundua dalili za mgonjwa.

Dawa za sanduku la huduma ya kwanza zaweza kupatikana kwenye hospitali za serikali kwa maombi rasmi au maduku yanayojihusisha na dawa baridi za binadamu.

YATENDEKAYO KATIKA KITUO CHA HIKING CHA MWISHO.

Baada ya kufika eneo la mwisho fanyeni yafuatayo: -

i. Wimbo uimbwe (Kitabuni au kwaya)
ii. Ombi lifuate
iii. Somo fupi linalokazia kusudi la Hiking dk.5
iv. Kuwe na vipindi mbalimbali vya kujifunza nishani, hasa za viumbe hasili kama buibui, kipepeo, mjusi(reptilia) n.k zile zinazohusu mazingira mliyopo.
v. Wana Hiking wafundishwe juu ya taabu ya Yakobo itakayowapata watu wa Mungu watakapokimbilia porini.
   Masomo yote haya wapewe walimu wenye ujuzi na waandaliwe mapema. Kila somo ni dk.40 tu.
vi. Baadae wanahiking wagawanywe kwenye vikosi vya watu 10-15. Hii hutegemea idadi ya wanahiking waliopo, kwa ujumla, wagawanywe katika makundi makubwa maana. Kila kundi lapaswa liwe na mwenyekiti na katibu. Kundi moja lielekee kaskazini, lingine kusini, lingine Mashariki na lingine magharibi.
   - Kazi itakayofanywa na makundi haya ni kuchunguza yafuatayo: -
   a. Mpango wa mawe ulivyo kama ni sehemu yam awe kutegemea na eneo
   b. Aina mbalimbali za miti na mito ya asili iliyopo.
   c. Sura ya nchi milima, mabonde, mmomonyoko, magema n.k
   d. Aina za wanyama na wadudu waliopo.
   e. Miti mbalimbali au mimea ambayo ni dawa
   f. Miti mbalimbali ambayo ni sumu.
   - Chochote watakachokiona ni cha pekee wachukue taarifa zake.
   - Ikibidi wachukue na mfano wa kuonyesha (sample)
   - Kazi hii ifanywe kwa muda wad k.20 hadi 30 tu.
   - Baada ya hapo filimbi itapigwa na makundi yote yatarejea tayari kutoa taarifa.

TARATIBU ZA UTOAJI TAARIFA.

Taarifa hutolewa na mwenyekiti wa kikosi kwakumkaribisha katibu, katibu ataanzakwa: -

a. Kuelezea uelekeo waliokwenda.
b. Kutanbukisha wana timu/kikosi.

c. Kuelezea wale waliyoyaona na kuonyesha mifano

UTOAJI MAKSI/ALAMA.

Viongozi watasaidiana kutathimini na kutoa maksi/alama.Vigezo vifuatavyo viangaliwe: -

i. Kujieleza –Lugha yake inasikika vizuri na kueleweka.
ii. Namna anavyosimama
iii. Mwonekano wake -ni wa furaha au huzuni na kwa nini?
iv. Mpangilio wake -je, Unaleta mantiki?
v. Uzito way ale yaliokusanywa. Namna walivyojishughulisha.

Maksi/alama zitolewe kwa kundi la kwanza hadi la nne.

Baadae wanahiking hurejea nyumbani, si lazima kufuata njia ile ile wakati wa kurudi.

Ikiwa viongozi watafuata taratibu hizi, Hiking itakuwa moja ya burudisho la kufaa na yenye manufaa makubwa katika miili yetu na kanisa hata jamii kwa ujumla.